https://dspace.org/

# Kimonro cha Mvuli asahau uume wake nrowa ni jamaa kinavowasilishwa katika Utendi wa Ramani ya Maisha ya Ndoa (Mume): Uchanganuzi Kifano

**Karama, Mohame**

**2023**
East African Journal of Swahili Studies
: https://doi.org/10.37284/2707-3475

Karama, M. (2023). Kimonro cha Mvuli asahau uume wake nrowa ni jamaa kinavowasilishwa katika Utendi wa Ramani ya Maisha ya Ndoa (Mume): Uchanganuzi Kifano.

Downloaded from a DSpace repository. https://dspace.org/

**East African Journal of Swahili Studies**
eajss.eanso.org
**Volume 6, Issue 1, 2023**
**Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475**
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# Kimonro cha Mvuli asahau uume wake nrowa ni jamaa kinavowasilishwa katika Utendi wa Ramani ya Maisha ya Ndoa (Mume): Uchanganuzi Kifano

*Dkt. Mohameḍ Karama, PhD*[1*]

[1] Chuo Kikuu cha Kabianga, S. L. P. 2030 – 20200, Kericho, Kenya.
[*] ORCID ID: https://orcid.org/0000-0003-2341-9966; Barua pepe ya mawasiliano: mkarama@kabianga.ac.ke

**DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1181**

**Tarehe ya Uchapishaji:**

*19 Aprili 2023*

**Istilahi Muhimu**:

*Ufupisho wa Ramanime, Masemezano, Ujamaa, Taharuki, Mjadala..*

**IKISIRI**

Katika ṭaaluma ya fasihi ya kiSwahili uṭeṇḍi maarufu uliyoṭafiṭiwa mno kuhusu masiyala ya nrowa, kazi na majukumu ya mke k̇a mumewe, ni ule wa Ṁanakupona. K̇a mara ya k̇anza, makala haya yanaangaziya uṭeṇḍi ṁengine ambao haujaṭafiṭiwa k̇a ṭafsili wenye kuraṭibu kazi na majukumu ya mume k̇a mkewe. Utendi wa Ramani ya Maisha ya Ndoa (Mume) uliyotungwa na Usṭadh Mahmouḍ Mau unampa mvulana wasiya wa kutumiya katika kufaulisha nrowa yake. Makala haya yaṇjaribu kudhihirisha elimu ya kiḍini na hekima ya ṭajiriba ya kimaisha aliyonayo mtunzi k̇a kumnasihi mvuli kuwa hakuna ukʰuu katika nrowa. Makala haya yakiongozwa na nadhariya ya Usemezano yamechanganuwa maudhui ya hekima ya mtunzi na kubainisha kuwa: k̇enye mukṭadha wa nrowa mke na mume wanasemezana si wao peke yao bali na jamii k̇a ujumla; kuna mabaḍiliko ya maana ya maneno kila kukicha basi na maana ya uume piya inabaḍilika kila kukicha; na ṁishowe, maana inayokuja baaḍa ya kukaa nrani ya maisha ya nrowa huwa ṭafauṭi na ile ilozoweleka. Makala haya yanahiṭimisha kuwa mtunzi aliṭaka kumfunza mvulana na msichana kuwa maisha ya nrowa ni ya watʰu wawili lakini majukumu zaiḍi yanaṁangukiya mume katika kufaulisha nrowa yake. Isiṭoshe, uṭeṇḍi huu unamkazaniya mume amsome mkewe kila siku kila saa ili aweze k̇idhibiṭi nrowa. Naṭija ilopatikana k̇a kuushughulikiya uṭeṇḍi huu ni kubaḍilisha nadhari katika ṭaaluma za kiSwahili na kijinsiya k̇a k̇angaziwa sana Ṁanakupona na kuṭoṭafiṭiwa ṭʰeṇḍi nyenginezo haswa zinazotiliya maanani mtoto wa kiyume.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

**APA CITATION**

Karama, M. (2023). Kimonro cha Mvuli asahau uume wake nrowa ni jamaa kinavowasilishwa katika Utendi wa Ramani ya Maisha ya Ndoa (Mume): Uchanganuzi Kifano *East African Journal of Swahili Studies*, *6*(1), 101-118. https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1181.

**CHICAGO CITATION**

Karama, Mohameḍ. 2023. "Kimonro cha Mvuli asahau uume wake nrowa ni jamaa kinavowasilishwa katika Utendi wa Ramani ya Maisha ya Ndoa (Mume): Uchanganuzi Kifano". *East African Journal of Swahili Studies* 6 (1), 101-118. https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1181.

**HARVARD CITATION**

Karama, M. (2023) "Kimonro cha Mvuli asahau uume wake nrowa ni jamaa kinavowasilishwa katika Utendi wa Ramani ya Maisha ya Ndoa (Mume): Uchanganuzi Kifano", *East African Journal of Swahili Studies*, 6(1), pp. 101-118. doi: 10.37284/jammk.6.1.1181.

**IEEE CITATION**

M. Karama, "Kimonro cha Mvuli asahau uume wake nrowa ni jamaa kinavowasilishwa katika Utendi wa Ramani ya Maisha ya Ndoa (Mume): Uchanganuzi Kifano", *EAJSS*, vol. 6, no. 1, pp. 101-118, Apr. 2023.

**MLA CITATION**

Karama, Mohameḍ. "Kimonro cha Mvuli asahau uume wake nrowa ni jamaa kinavowasilishwa katika Utendi wa Ramani ya Maisha ya Ndoa (Mume): Uchanganuzi Kifano". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 6, no. 1, Apr. 2023, pp. 101-118, doi:10.37284/jammk.6.1.1181.

## UTANGULIZI

Kauli ni chombo hayi katika makawaṇḍa ya mawasiliyano ambapo hwingiliyana na mazingira yake na k̇angaza maana inayokusuḍiwa k̇a kushirikisha wanajamii wot̩ʰe. Kulingana na Bakhtin (1981, uk. 262) kauli ina viyashiriya vingi: usuli, mapisi, uṭamaḍuni, niya, athari za kisajili vinavojumuika pamoja ili k̇athiri maana ya ṭamko. Zaiḍi ya hilo, maana ya kauli hujiṭokeza k̇a mchanganyiko wa nrimi zot̩ʰe katika lugha na hakuna ainaṭi moja iṭakayojinaki kuwa bora zaiḍi kuliko nyengine katika kupa maana ya kauli.

Bakhtin (1981, uk. 272) anayeleza kuwa k̇ingiliyana k̇a ainaṭi za lugha mambo yanayodhihirika ni k̇amba maneno katika lugha huwa katika masemezano na wakaṭi na mahali yanapoṭaka kutumiwa; haiwezekani kuchukuwa neno kikamusi na liwafiki matumizi mamoja wakaṭiwot̩ʰe mahali mwot̩ʰe. Sifa nyengine ni k̇amba maana ya neno haiwi nriyo ya ṁisho k̇a sababu nrani ya neno lenyewe kuna nguvu za kʰani-kutanishi na kʰani-ṭawanyishi kuṭokana na ṭaharuki iliyosababishwa na ṁingiliyano wa vipera ṭafauṭiṭafauṭi katika mukṭadha mmoja wakaṭi wa maongezi. Kuṭokana na maneno kuwa katika masemezano na ujamaa (haina mnasaba na iṭikaḍi ya kiMaksi) katika jamii nzima ya mawasiliyano na ṭaharuki iliyopo basi husababisha kila maana inayomulik̇a na neno huwa imepeta kiḍogo (uk. 299)—ni ṭafauṭi na ṁanzo lilivotumika. Yaani, kila siku kila saa neno linapata maana mpya (uk. 291) na k̇a umaharajani(hali ya kuṭweza cheyo) huu mtumiyaji wa neno fulani huwa nriye mjuzi wa maana ya neno hilo (uk. xix). Mambo mane haya: usemezano, ujamaa, ṭaharuki, na upete wa maana ya neno nriyo yaṭakayojenga fikra zetu kuchanganuliya miyonroko ya mume katika nyumba yake kama ilivowasilishwa katika *Utendiwa Ramani ya Maisha ya Ndoa—Mume* (soma *Ramanime*) uliyotungwa ni Usṭadh Mahmouḍ Ahmaḍ Abdulqadir (soma Usṭadhi k̇a kufuwata wanavoṁita wanaṭi wa Amu, Lamu).

Katika ḍori la ṭaaluma ya kiSwahili kuna t̩ʰeṇḍi kadhaa zilizoangaziwa zaiḍi miyongoni ṁazo ni uṭeṇḍiwa Siri li Asrari, Hamziyya, Tambuka nazo ni za kabla ya 19 K. Wakaṭit̩ʰeṇḍi hizi zilihusu maisha na piya misafara ya kivita alivopigana Mtume Muhammaḍ, uṭeṇḍi uliyokiyuka kaida hii ni Uṭeṇḍi wa Ṁanakupona. Umekiyuka k̇a sababu haukumkhusisha Mtume Muhammaḍ pekee wala vita alivojiṭoleya kupiganiya haki ya wanyonge bali unahusu maisha ya nrowa nrani ya nyumba ya

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1181

ṁisilamu ukimlenga mke (Chiraghdin, 1987) na juzijuzi Wandera-Simwa (2021). Ṭʰeṇḍi nyenginezo hususani za mke katika nyumba yake ni *Manukato ya Wambeja* (Nabhany, h.t), *Ramani ya Maisha ya Ndoa—Mke* (Abdulqadir, 2004; Ankal Nassim, 2013), *Wasiya wa Mabanati* (Raia & Vierke, 2023). Ṭʰafiṭi na ṭʰeṇḍi zoṭʰe hizo zimeyakisi kazi na majukumu ya mke katika masikani yake. Mpaka sasa ṫaṇḍikapo makala haya, k̇a ufahamu wetu, hakuna uṭeṇḍiuliyoṭafiṭiwa unaohusu kazi na majukumu ya mume katika masikani ya mke wa kiSwahili. Haṭa Utendi wa Hapo Zamani za Yana uliyotajwa katika *Ramanime* ubeṭi 5 na Raia & Vierke (2023) umetaja ṁamala wa maisha yoṭʰe lakini si k̇a kukhusisha kazi na majukumu ya mume k̇a mkewe. Dhana inayojiṭokeza katika ṭaaluma nzima ya kiSwahili na ya jinsiya ni k̇amba mtoto wa kike pekee nriye anayesisitiziwa zaiḍi katika ṭʰafiṭi za kinrowa na kughafilika na mtoto wa kiyume—jambo Momanyi (2019) analolalamikiya na kufuṭu ni kosa—ambapo ṭangu azali waSwahili walikuwa na kʰumbi ambako walipelek̇a kufunzwa masiyala ya nrowa na umasikani (Cory, 1947; Mbaabu, 1985). Isitoshe, tunadhamiriya k̇angaza suwala la siyasa ya lugha (Biersteker, 1991; Mazrui & Njogu, 2022) katika nrowa ya kiSwahili jambo ambalo halijaṭafiṭiwa kwa kina na mapana yoṭʰe.

Makala haya yanaushuwa, k̇enye ṭaaluma ya kiSwahili, uṭeṇḍi huu unaowahusu wanaume katika masikani yao ya nrowa na yanajaribu kuonesha namna mvuli aṭakavookoleka k̇enye bahari kʰuu ya uliṁengu wa nrowa. Lengo jengine ni kwonesha namna mtunzi wake anavogeuza maana ya uume katika masikani yake na kuufanywa kufu moja na mshirika-ṁenza—mkewe—katika nrowa yao baḍala ya vyeo vilivowasilishwa na Ṁanakupona (Werner & Hichens, 1934) au jamii ya waSwahili, mume juu mke chini. Makala haya yaṭashikiliya hoja kuwa, kama vile neno halina mashiko ya kukitisha maana moja, uume nawo katika nrowa na masikani hugeukageuka bila kukitisha msimamo mmoja nani ni mṭawala wa nyumba na mambo hivo kufaulisha nrowa. Maelezo yetu yaṭaṭokana na uchanganuzi wa maudhui ya uume alivowasilisha Usṭadhi katika maṭini ya *Ramanime*. Katika makala haya uume ina maana ya 'hali ya kuwa ṁanamume kijinsiya (kiAfrika-jadi [Mazrui & Shariff, 1993, uk. 6]) yenye chembe za ubabe haṭa kama haudhihirishwi kimatenro' na wala siyo kama alivomaanisha Mwamzandi (2018) k̇amba ni tupu ya mbele (zubu)—kiyungo cha ṁili. Hali kadhalika, masikani iṭamaanisha mahali *home* wanapoishi wanarowa na piya kuchukuwa fasiri ya kiArabu ya 'utulivu' (Baalbaki, 1995) na wala si jengo ṭu. Aidhan, mvuli na mvulana ziṭatumika sawiya k̇a maana ya barobaro aloṭayari kuwowa; na mume k̇a maana ya ṁanamume alofunga nrowa na mke. Tuṭatumiya /t ṭ ṭʰ tʰ ḍ ṇ ṫ ṁ k̇ ġ ṗ ṇḍ/ kuwakilisha /t d n tw mw kw gw pw nd/ za kiSwahili Sanifu kama alivopeṇḍekeza Karama (2022), isipokuwa madonroo ya maṭini inayoshughulikiwa.

## Ufupisho wa *Ramanime*

Uṭeṇḍihuu ulitungwa baada ya kutungwa *Utendiwa Ramani ya Maisha ya Ndoa—Mke* (2004) kama inavotaja *Ramanime* ubeṭi 2. Katika ubeṭi huwohuwo uṭeṇḍi wa k̇anza uliwahusu mahavule na wa pili wawahusu wavulana lakini katika ubeṭi wa 251, ambawo nriyo wa ṁisho, Usṭadhi anasema amewakusudiya woṭʰe wawili: wavulana na wasichana. Haswa ni uṭeṇḍi wa kipekee tunavojuwa sisi uliyoaṇḍik̇a kuwanasihi wavulana kuhusu namna ya kukaa nrani ya masikani yawo waṭakapoowa. Hapana shaka, na si makosa kama asemavo Mohamed (2016) katika Dibaji yake k̇amba kazi za kifasihi hwingiliyana na k̇athiriyana kimaudhui na kifani, k̇amba Usṭadhi aliyathiriwa na kazi za kale za washairi wakuɓa kama Ṁanakupona (pengine Usṭadhi alipata ilihamu kuṭoka nyumba yake iliyoko jirani naye Mtaṁini, kisiwani Amu). Kama alivofanya Ṁanakupona hapo kabla, Usṭadhi naye alimshika shikiyo ṁanawe wa kiyume Yahaya kuhusu namna ya kuishi na mkewe. Japo uliyaṇḍikiwa Yahaya lakini piya uliwachanganya wavuli woṭʰe k̇a urejelezi wa ubeṭi 1, 2

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1181

/Namwandikiya Yahaya... Na hini nimeiunda...wavulana kuwambiya/.

Uchanganuzi wetu umekuja kupata nyasiya za makumbo kumi, kama amri za Nabii Musa, ambazo mtunzi aliṁaidhi ṁanawe kuhusu maisha ya nrowa. Alimnasihi ajuwe: vipimo va kujichaguliya mke; mipaka ya k̇icheza harusi yake; kupamba nyumba yake na mkewe; k̇amiliyana na mkewe katika mambo ya kawaiḍa; namna ya kufanya ngono naye; hali ya ṁili wa mkewe anapokuwa k̇enye hedhi na mimba; uzito wa ṭalaka; kaṭu asiyengeze mke; kuwaheshimu wak̇eze na namna ya kuṭangamana na wajomba, mashangazi, mashemegize wa kike; mikakati ya kutatuwa utesi unapozuka. Usṭadhi anaona kuwa akiyashika mambo haya ṁanawe aṭafaulu katika nrowa yake.

Kifani *Ramanime* umejiṭosheleza k̇a kuwa na sifa za kipera cha uṭeṇḍi: mishororo mine, kina kimoja kila mshororo na bahari, mizani nane kila mshororo, utangulizi na kihiṭimisho. Lugha yake ni ya kiAmu iliyochanganyikana na kiṬʰikuu kiḍogo, kuna utohozi wa maneno ya kiIngereza (boya, zigizagi, lojingi, vito, fesheni, kaseti) na yaeleweka k̇a wepesi. Ametumiya jazanra za boya, ṭabiya ni tʰaa au ni ṭʰomomo, ugomvi ni kibiriṭi, ṭeṭe, kuni, au pamba na moto wakaṭimatatizo yanapozuka, mvuli k̇iṭa fahali, uliṁengu wa nrowa ni ṭamu na uchungu na kadhalika. Mtunzi hakuwacha kutumiya vihisishi, tashṭiṭi, udamisi katika kumkemeya mume kuhusu ṭabiya mbaya ya kumrukiya mkewe. Lugha hii ya kiṭamathali inaufanya uṭeṇḍi uwe ṁanana k̇enye masikizi ya msikilizaji ambayo nriyo jihazi apeṇḍeleyayo mtunzi kuufikisha ujumbe wake kuliko kuwa ni kiṭabu.

Nukusani ya *Ramanime* ni k̇epuka kutupa ṭarehe na jina la mtunzi katika uṭeṇḍiwenyewe kama kaida ya ṭʰeṇḍi nyenginezo (Shitemi, 2010) zijulikanazo mfano *Siri li Asrari* (Bwanalemba, 1662). Pengine mtunzi alighafilika au pengine ni mtinro kama *Manukato ya Wambeja* tuliyoutaja hauna ṭarehe lakini una jina. Ṭarehe na jina la mtunzi ṫapata katika dataelezi ya nakalakar alotukabidhi mtunzi ṁenyewe Usṭadhi tulipokuwa tukifanya kazi Research Institute of Swahili Studies of Eastern Africa (RISSEA), Lamu mnamo 2007. Katika nakala hiyo dataelezi inasema kuwa *Ramanime* ulitungwa na Ustadh Mahmoud Ahmad Mahmoud (sic)(MAU) wa Lamu, Kenya katika ṁaka wa 2004 na ulipakiwa k̇enye wavuti wa zanzinet (hatukuupata ṭena wavuti huu tulipoṭafiṭi mtanraoni majuzi) na Saleh Barkey mnamo Februwari 2005. Haṭa k̇enye wavuti wa Jamiiforums.com (https://www.jamiiforums.com) maelezo hayahaya ya ṭarehe na mtunzi yanapatikana hivihivi lakini mpakizi wa uṭeṇḍik̇enye mtanrao huwo hakutajwa. Haṭa hivo, *Ramanime* umetajwa kuwa ulitungwa 2006 katika kazi za Abdulkadir & Frankl (2013), na Raia & Vierke (2023). Hakuna ubishani katika jina la mtunzi au mmiliki wa uṭeṇḍihuu maana imehakikishwa na kazi zilizokuja baaḍaye (ambapo Usṭadhi ni mmoja wa wachangizi wa kazi hizo) kuwa *Ramanime* ulitungwa na Usṭadhi na nakala tulonayo tulipawa na yeye na si kupitiya k̇a mkono wa mtʰu ṁengine. Fauka ya hayo, lakabu ya 'Mau' katika ushairi wa kiSwahili yajulikana kuwa ni ya Usṭadhi. Ama kuhusu ṭarehe tuṭachukuliya kuwa 2004 nriyo sahihi k̇a sababu nriyo iliyomo k̇enye nakalakar, na pili, dataelezi ya zanzinet inaonesha mpaka jina la mpakizi na ṭarehe ulipopakiwa k̇enye wavuti huwo. Alhasil, ṭashwishi ya ṭarehe haidhuru kitʰu katika suala letu la maudhui, ni ṭanabahisho ṭu lakini mmiliki ni tujuweṁaṇḍishi ni Usṭadhi.

Kaiḍa nyengine ya uṭeṇḍi ambayo *Ramanime* iliyepuka, ni kukosekana kihiṭimisho ṁishoni ṁake. Hakuna ile kaiḍa ya ufupisho wa msisitizo wa hoja na ṭasnifu ya mtunzi katika kihiṭimisho, ni kama kilipachik̇a k̇a kukata muwala wa mawazo anayozungumziya. Bado kuna masiyala mengine ya nrowani, sisi ṫadhani, ambayo Usṭadhi angeyagusiya kama: kufagiya, kosha vombo na choo, kumfuliya kujifuliya nguwo, kumpikiya, kumsomesha Kuruwani, kumnunuliya nafaka, kuṁangaliya anapokuwa mgonjwa. Alakulihali, ni uṭeṇḍiunaosṭahiki sifa na wazungumziya mambo ya sasa unaofaa kutambulikana mbele ya

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1181

ṭʰeṇḍimaarufu katika fasihi ya kiSwahili na uliṁengu.

## UCHANGANUZI

Uchanganuzi wetu umejiyegemeza k̇enye viyashiriya vine: masemezano, ujamaa, ṭaharuki katika kauli, na upete wa maana nrivo viṭakavotumika kudhihirisha ainaṭi za lugha zoṭʰe zipatikanazo na zinavochangizana katika *Ramanime*.

### Masemezano

Tumesema ṁanzo kuwa kauli katika jamii nzima ya mawasiliyano imo katika masemezano na mazingira inamotumika na k̇amba kauli hizi hwathiriyana na kusemezana kuṭokana na mukṭadha (mapisi, usuli, uṭamaḍuni, na sajili) unaojengwa. Hivo katika kiyelelezo cha mawasiliyano anachopendekeza Bakhtin (1981) kuna mpokezi hayi anayeathiri usemaji wa msemaji na mbinu hii nriyo inayofaulisha kuwasilisha maana halisi siyo maana ya kijuujuu. K̇a minṭarafu hiyo basi, *Ramanime* inadhihirisha mtunzi anampa mvulana naswaha kama alivofanya babake mzazi Bwana Ahmad Abdulqadir. Usṭadhi anatufahamisha hivi:

*3. Na asili ya kwaandika*

*Nahisi wana wataka*

*Baba piya kadhalika*

*Mimi alinandikiya.*

*4. Baba bwana Ahmadi*

*Atamjazi Wadudi*

*Kwani alijitahidi*

*Kunandikiya wasiya.*

Juu ya k̇amba aliyaṇḍikiwa ni babake Bwana Ahmaḍi katika uṭeṇḍi wa Hapo zamani za yana (ubeṭi 5) kumuusiya kuhusu nrowa lakini anaṫambiya k̇amba jambo hili la kunasihiwa ni la ‘kuhiṭajiwa’ ubeṭi 3 k̇amba wavulana wanafaa wapawe wasisubiriwe kuomba naswaha.

Jambo jengine ambalo lajiṭokeza awali ya mambo ni nafasi ya ḍini katika mfanyiko mzima wa nrowa. *Ramanime* imeweka mbele suala la ḍini na athari yake katika maṭeuzi yoṭʰe anayoyafanya mvulana ṁisilamu anapoṭaka kuwowa. Usṭadhi anatʰongowa:

*10. Mwanangu ukiazimu*

*Kuowa kwanda fahamu*

*Kuteuwa ni muhimu*

*Ni amri ya shariya.*

*11. Mtumi alibaini*

*Akatwambiya owani*

*Mwanamke mwenye dini*

*Mungu tawabarikiya.*

Tuṭaona katika beṭi hizo kuwa kuṭauwa kuko lakini k̇aṭokana na amri ya Shariya ya Mungu (ya kiIsilamu) ambayo imewek̇a wazi na Mtume Muhammaḍ. Mke afaaye kuwowa ni yule ṁenye ḍini. Japo katika beṭi zinazofuwata hizi zayeleza kuhusu aowe ṁanamke ṁenye pato, nasaba, uzuri lakini sharuṭi kʰuu ni awe na ḍini. Tuṭaona kuwa Usṭadhi hakuṁambiya sharuṭi hili k̇a kusoma ṭu katika viṭabu va ḍini bali anaṁeleza kijana wake Yahaya piya yanaṭokana na ṭajiriba yake ya kimaisha na masomo alosoma kuṭoka k̇a walimu wa hekima ya maisha (ubeṭi 7).

Tukiwa baḍo k̇enye masuwala haya ya elimu na utambuzi mtunzi anamshauri mvuli atumiye na akili yake au saa nyengine apime mambo k̇a mizani ya kiyasi. Asitumiye elimu ya maḍarasani na kimaisha lakini kuna yeye na akili yake piya lazima azungumze nayo ili kujuwa uwamuzi aṭakaoufanya kuhusu mambo katika masikani yake. Anaṁambiya:

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1181

*33. Moya moya sitoweza*

*Kutondowa kukweleza*

*Nimekupa muangaza*

*Wa ndiya kufuatiya.*

*34. Nimekupa ni kiyasi*

*Kitumyie nawe basi*

*Kwa mangineyo kukisi*

*Kwa mizani kutumiya.*

*131. Mke kikukasirisha*

*Jaribu kuyikumbusha*

*Piya hukufurahisha*

*Mezani hini tumiya.*

Baaḍa ya kuṁeleza kuhusu jukumu la ḍini katika uṭeuzi wa mke na namna ya kusherehekeya harusi, mtunzi anaṁachiya atumiye na akili yake pamoja na k̇akisi k̇a mizani ya mifano aliyompa. Hili laonesha kuwa mtunzi anamṭaka kijana wake asemezane na akili yake ili apate maarifa zaiḍi kuhusu maisha ya nrowa. K̇a hivo, kuna masemezano baina ya Usṭadhi, kijana, na upimaji wa mambo k̇a akili (maarifa) ambayo yaṭajisaili na kujaḍiliyana wenyewe k̇a wenyewe mpaka muwafaka upatikane.

Masemezano tuliyoyaangaziya mpaka sasa ṫaweza kusema ni ya kiyalama: yaṭokana na viṭabu va kiḍini, saikolojiya k̇a kutumiya akili. Lakini mtunzi ameonesha masemezano ya kimatenro haswa—kuna wahusika wawili na wanasemezana kama mazungumzo halisi. K̇anza anamjulisha mvulana kuwa ukiwa na mke ujuwe huyo ni mt$^{h}$u wa pili nyumbani; si peke yake ṭena. Pili, anaṁambiya amtengenezee na 'juk̇aa huru' la kuweza na yeye kusema. Mtunzi anasema:

*116. Mke wako si kivuli*

*Bali ni mtu wa pili*

*Una na yake akili*

*Una na alozoweya.*

*118. Muatiye makawanda*

*Anene anolipenda*

*Na kwa huja kikushinda*

*Siwe vito tatumiya*

Katika beṭi hizo mvuli anashauriwa aṁekee mkewe kiwanja (nafasi) cha yeye kusema analolifikiriya ni sawa. Mbali ya nafasi apawe na uwezo wa kuṭowa rayi katika mambo yanayohusu masikani yao. K̇a hivo mandhari ya mapokezano ya mawazo yanawek̇a ili wenye nyumba wajaḍiliyane, washauriyane. Mfano ṁengine wa masemezano haya ya ana k̇a ana yanaonekana katika uṭeṇḍimzima ambapo Usṭadhi anamsemeza ṁanawe Yahaya. Anasema katika ubeṭi 1 /Namwandikiya Yahaya/, ubeṭi 10 /mwanangu ukiazimu, Kuowa kwanda fahamu/ na ubeṭi 194 /Nimekwambiya Yahaya/.

Venginevo, tunakumbana na masemezano ya kiishara ya viungo va ṁili. Msemezano huu unajiṭokeza katika shughuli anayoiyita k̇a tasifida 'siri ya siri' ubeṭi 143 na 'mambo ya tini kwa tini' ubeṭi 145, au k̇a uwazi 'ngono' ubeṭi 159. Masiyala haya Usṭadhi ameyaelezeya k̇a urefu (beṭi 95-106 na 151-160) k̇a sababu anasema 'chanzo cha majumba [masikani] kuvunjika ni wat$^{h}$u kuṭoṭoshelezana katika ngono' (ubeṭi 159), na wakiṭoshelezana basi ukorofi nrani ya nyumba [masikani] huonroka na mafarakano mengine wananrowa huvumiliyana (ubeṭi 160). Hapa tunadhihirishiwa jambo la kusemezana katika haṭa shughuli ya kitanra cha nrowa: anatuonesha namna kuchezacheza baina ya wananrowa kabla ya kuunrama yaṭakiwa mume afanye vipi. *Ramanime* unafafanuwa kuwa mbinu bora na yenye nguvu ni 'kutumiya mato (macho)'. Beṭi hizi zinasisitiza matumizi ya lugha ya macho (kiishara) katika kuvuta hisiya za wananrowa ili wasemezane. Mtunzi anaṭamthilisha hivi:

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1181

*95. Na faragha ukipata*

*Mbee yako kikupita*

*Usiwe utamuata*

*Mkono kumpekeya.*

*96. Mshike wake mkono*

*Wala simkaze mno*

*Hutosha nukuta tano*

*Ujumbe kumpekeya.*

*97. Kiwa amekukabili*

*Siitiye mashughuli*

*Inuwa yako mawili*

*Na yake kumwelekeya.*

*98. Wata mato yafumane*

*Katiti yangaliyane*

*Kwa ulimi usinene*

*Lugha ya mato tumiya.*

*99. Mato yana lugha tamu*

*Hunena mukafahamu*

*Mato kiungo muhimu*

*Cha huba kupaliliya.*

*100. Mato yana kuu siri*

*Na mara hukuadhiri*

*Kakutoleya khabari*

*Moyoni uloziwiya.*

*101. Hili nimenena sana*

*Ni muhimu naliona*

*Wala gharama halina*

*Na si kazi kutumiya.*

Katika kuziyamsha hisiya za ngono mume anapopata faragha (upekee) basi asiṁache mkewe kumpita bila haṭa kumḍara. Afanye hivo k̇a kumshika mkono na kuubinya kiḍogo kumpelekeya ishara. Mke anapoṁangaliya mumewe basi na mume naye asijitiye hamnazo aregeshe ishara ile k̇a macho. Macho yakutane yakit$^{h}$e k̇angaliyana na hapo kila kit$^{h}$u kiṭakuwa sahali mpaka kufikiya kitenro chenyewe cha kujamiiyana. Na mtunzi kuṭokana na utambuzi wake hili si kazi ngumu kupata uṭakacho k̇a ishara ṭu.

Katika masemezano haṭa akawa msikilizaji amenyamaa baḍo anaṁathiri msemaji k̇a sababu nrani ya ukimya wake nriyo msemaji huchaguwa aina ya jawabu aṭakayoṁambiya msikilizaji; ukimya piya ni aina ya usemaji. Mfanyiko huu tunauwona katika *Ramanime* wakaṭi mume anapokumbana na mke ni matata (ni mzinifu) basi ampeleleze mkewe k̇a siri bila kuṭamka neno wala kufanya ṭuhuma mpaka ayakinishe k̇amba mambo ni k̇eli basi hapo ṭena asimtajiye dhamiri yake bali aṁepuke kimyakimya ili kusiṭiri mambo hayo ya aibu yasiṭoke nje. Mtunzi anamfunza ṁanawe hivi:

*231. Na fununu ukipata*

*Kuwa mke ni matata*

*Siinuke na kuteta*

*Kwanda zidi kwangaliya.*

*232. Simtukuliye dhana*

*Kwa kuwa waja hunena*

*Hilo ni khatari sana*

*Mayutoni takutiya.*

*233. Iziwiye usubiri*

*Uhakikishe khabari*

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1181

*Tena ufanye kwa siri*

*Pasi na kupija mbiya.*

*234. Ikiwa umetosheka*

*Hilo ni yambo hakika*

*Kwa taratibu epuka*

*Bila sababu kutaya.*

*235. Sitaye yako sababu*

*Utazidi kuharibu*

*Zitatangaa aibu*

*Na si wema kueneya.*

Ṁane anafunzwa namna ya kufanya uchunguzi aṭaposikiya kuwa mkewe ni ṁenye 'jicho la nje'—ni ṁasharaṭi. K̇anza asifanye fujo wala kumchukuliya dhana mbaya. Afanye upelelezi wake na aṭakapothubuṭisha basi aṁache polepole bila ya kupigizana kelele na wat$^{h}$u wa nje kupata habari ya aibu kama hiyo. K̇a hivo, Usṭadhi anampa mbinu za kutatuwa matatizo yake k̇a salama na amani bila ya kufunuwa wazi yaliyomo moyoni ṁake. Akiṭahamaka bibiye aone mambo yashakuwa mabaya k̇a upanre wake k̇a sababu hakujuwa ule ukimya ulikuwa wasema nini.

**Ujamaa**

Mbali ya k̇amba kauli zimo katika masemezano piya maneno hwathiriyana na maneno mengine katika mt$^{h}$ongoo mmoja wa mawasiliyano na kufanya kauli ziwe katika hali ya ujamaa. Au, k̇a mfano, msemaji anaṭaka kutumiya sajili fulani wakaṭi wa kusema k̇ake basi ni mukṭadha wa hali hiyo husababisha msemaji aṭeuwe ainaṭi ya lugha ziṭakazowafiki sajili hiyo. Jambo hili la ujamaa Usṭadhi amelisisitiziya katika *Ramanime* na amelidhihirisha k̇a uwazi wa maṭangamano ya mvuli na mkewe na amelifanya kama nriyo ṭabiya njema mume kujipamba nayo.

Mtunzi anaanza mara moja kumfunza ṁanawe kuhusu upambaji wa nyumba (jengo) yake. Anaṁambiya lazima aifanye nyumba yake yapeṇḍeza k̇a kujaza kila aina ya vit$^{h}$u vizuri: samani, firashi na nakshi nyenginezo bila ya kukusuru k̇a sababu ya ubahili. Ajiṭolee amtiliye kila kit$^{h}$u mkewe ili na yeye asiyone va wengine akaṭamani vao. Ṭena asifanye k̇amba mkewe, pengine, k̇ao hakuna vit$^{h}$u hivo basi akamsuta k̇a kuṁambiya, 'waṭaka hivo na k̇etu au k̇enu hakuna'. Mtunzi ananasihi kuhusu kupamba nyumba:

*35. Na wewe kwako nyumbani*

*Siifanye mno duni*

*Kuwa mtu wasitani*

*Kwa mapambo kuyitiya.*

*52. Mtiliye mke wako*

*Zitu kwa kadiri yako*

*Ikiwa nafasi iko*

*Sibane ukaziwiya.*

*53. Iwe maridadi nyumba*

*Na kwa zitu kuipamba*

*Fesheni ambazo kwamba*

*Kama yeye hutumiya.*

*54. Mtiliye kula kitu*

*Awe kama wende watu*

*Simwambiye mimi kwetu*

*Haya sikuyazoweya.*

*55. Akiwa mbwa minazini*

*Ukimueta muyini*

*Simuwate kutamani*

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1181

*Za wende kishuhudiya.*

*57. Simwambiye zitu hizi*

*Kwenu kupata huwezi*

*Kwenu ni kama kizizi*

*Hukuona mazuliya.*

Mvuli anawaidhiwa ajaribu k̇a uweza wake kuipamba nyumba yake k̇a kila kizuri ili mkewe asiṭamani k̇a wenziwe anapowaṭembeleya mak̇ao. Asifanye ubahili au kufanya jeuri k̇amba k̇a kina mke hakuna, k̇a sababu ni wa mashambani, basi huku k̇ake hana haja ya kuwa navo. Wala asimsimbuliye k̇amba k̇awo ni kubovu haṭa kushinra alipo sasa.

Katika mfululizo huu wa mapambo Usṭadhi anamshauri kama alivoipamba nyumba yake basi na yeye mume piya aipambe haiba yake. *Ramanime* unaṁambiya mume ajipambe na kujiweka mzuri k̇a sababu hilo humfurahisha mkewe. Apeṇḍa amwone mumewe mbele za wenzake naye apeṇḍeza na wala siyo kujiṭupa k̇a kuvaa 'magozi' (magwanra ya kazini) akiṭembeya nayo mitaani mpaka nrani ya masikani yao. Anasema mtunzi:

*73. Na wewe upande wako*

*Ipambe kiyasi chako*

*Bora usivunde miko*

*Khatiyani ukangiya.*

*74. Kuwa mtu maridadi*

*Utunge yako jasadi*

*Hata kufukiza udi*

*Ukiweza si khatiya.*

*75. Iweke uwe nadhifu*

*Sionekane mchafu*

*Hini ni sunna tukufu*

*Ya tuṁa wetu nabiya*

*77. Ikiwa wafurahika*

*Mkeo akipambika*

*Yuwa na yeye hutaka*

*Nawe uwe huvutiya.*

*79. Naye piya hutamani*

*Akikuona ndiani*

*Uwe nawe hisabuni*

*Penye watu utangiya.*

*80. Au kiwa yako kazi*

*Kutenda haya huwezi*

*Wisapo vuwa magozi*

*Sivae kutembeleya.*

Mtunzi anamfunza mvuli wake ajiweke nadhifu, ajipambe apeṇḍeze k̇a nguwo safi na manukat$^{h}$o mazuri awe mṭanashaṭi mbele ya wenzake na k̇a mkewe zaiḍi. Hilo haliṭofurahisha wenzake ṭu bali piya liṭamfurahisha mkewe ajifakhiri moyoni k̇amba na mumewe piya ni 'mt$^{h}$u'. Tuṭaona k̇amba mbali ya upambe wa nyumba na mt$^{h}$u ṁenyewe piya apeṇḍeze.

Katika kikozi hichi cha kupaana maneno mazuri na kusifiyana basi hujenga maṭangamano mema k̇a sababu mke ahiṭajiya zaiḍi maoni ya mumewe juu ya jambo loloṭ$^{h}$e nrani ya masikani yake. Tuṭaona kuwa ujamaa huziḍi kushikana kuṭokana na kila mmoja k̇amiliyana na ṁenziwe k̇a uzuri. Mtunzi anamuusiya ṁanawe kuwa:

*83. Mno sana jitahidi*

*Kwa maneno maridadi*

*Wake hutaka zaidi*

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1181

*Yalo tamu kusikiya.*

*86. Mwanamke ahitaji*

*Kuvishwa la sifa taji*

*Kwa hilo kuwa mpaji*

*Usichoke kumwambiya.*

*89. Mwambiye umependeza*

*Kwa nyee kuzitengeza*

*Sina budi takutunza*

*Umshumu mara moya.*

*91. Kijifunga asumini*

*Au kikuba kitwani*

*Sichelewe kubaini*

*Neno lema kumwambiya.*

*92. Yaani kula wakaṭi*

*Mwambiye kitu katiti*

*Na kama bubwi siketi*

*Au duko tongo piya.*

*93. Piya mpe shukurani*

*Kwa shughuli za nyumbani*

*Mfano pilau hini*

*Mno umeipatiya.*

*94. Usichoke kumsifu*

*Kwa nyumba kuwa nadhifu*

*Na ukiona uchafu*

*Usiwe tamuukiya.*

Usṭadhi anamnasihi ṁanawe asiwache kumpa mkewe neno zuri kila saa na wakaṭi. Kusifiya mapishi yake, kujipamba k̇ake, kuiweka nyumba yake nadhifu asichoke kumsifu nrilo apeṇḍalo. Ṭena asijifanye kiziwi, kipofu au bubu asiseme loloṭʰe baaḍa ya kuona uzuri huwo. Na akikoseya mahali asiwe haraka kumkemeya.

### Ṭaharuki

Tulisema mbeleni kuwa maana ya kauli haibakii kuwa moja k̇a sababu kuna nguvu za kʰani-kutanishi na kʰani-ṭawanyishi zinazosababisha ṭaharuki kila mukṭadha ukibaḍilika na hivo kuzuwa kila saa kila siku maana mpya ya neno. Nriposana katika hali hii ya utulivu na mambo mazurimazuri basi Usṭadhi anamkumbusha ṁanawe kuwa /nyumba [masikani] si pepo/ ubeṭi 115; maisha ni tamu na utungu (beṭi 112 – 115). Ikishakuwa mambo ya masikani ni mabaḍiliko ya mara k̇a mara basi kitʰu cha muhimu anachofunzwa mvulana ni AMSOME MKEWE (msisitizo ni wetu) ubeṭi 172. Tumeweka k̇a herufi kubwa k̇a sababu kufuwata msemo 'kusoma hakwishi' na kushaḍiḍiya hoja yetu kuwa mume asahau yeye yuwajuwa. Mtunzi anaṁambiya hivi:

*172. Ni muhimu kula mume*

*Mke wake amsome*

*Kwa zipimo ampime*

*Siku zikikaribiya.*

*173. Ukisa kumfahamu*

*Uwate kumlaumu*

*Hili mno ni muhimu*

*Yataka kulizoweya.*

Mvuli anaambiwa ajishughulishe na kumsoma mkewe ili ajuwe mambo ya mkewe vilivo. Asome mabaḍiliko ya ṭabiya, ṁili, fikira, miyonroko wakaṭifulani na akishamjuwa awache na kumlaumu k̇a sababu ya baḍiliko lake kila baaḍa ya muḍa. Na elimu anayoṭanabahishwa huyu kijana ni ya hali ya kiṭajiriba zinazotʰukiya katika maisha.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1181

Msimamo anawokuja nawo mvulana aliyobaleghe ni k̇amba nrowa ni yake na anakuja na msimamo wa yeye yuko juu ya watʰu woṭʰe k̇a sababu ni cheyo alichopawa na jamii yenye k̇elemeya kuumeni. Lakini *Ramanime* unakuja kuṁonesha kuwa cheyo chake ni upili katika uṭeuzi wowoṭʰe anawoṭaka kuufanya. K̇a vile ḍini ya kiIslamu ni yenye kuṭawala maisha mazima ya muumini wake basi haṭa nrowa piya ina masharuṭi na mipaka yake ya kuzingaṭiwa. Ḍini inayoseṁa hapa si ḍini ya kibanriko cha jina la muumini bali ni ḍini iliyokitʰa moyoni yenye kwonekana na matenro mazuri ya muumini huyo pamoja na kuwacha makatazo ya Bwana Mola (ubeṭi 18). Kuṭoka uṭeuzi wa mke, kusherehekeya harusi yenyewe mpaka rafiki yake awe nani na wapi wakaṭi wa harusi hiyo, mavazi yapi avaye mkewe ḍini inakupa mipaka yake. Hivo iṭaonekana kuwa mvuli huyu ile maana yake kuwa nriye msimamizi, ṁelekezi na mṭawala wa nrowa yake haikubaliki mbele ya ḍini. Anamṭanabahisha ṁanawe hivi:

*11. Mtumi alibaini*

*Akatwambiya owani*

*Mwanamke mwenye dini*

*Mungu tawabarikiya.*

*18. Dini ninayoinena*

*Sikuwa nayo ni ina*

*Dini ni kwandama sana*

*Amri zake Jaliya.*

*27. Hafula za isirafu*

*Na za magoma machafu*

*Na kuwa tutu kwa ufu*

*Dini hayo huzuwiya.*

*39. Rafiki usimliche*

*Ni zaidi huyo mche*

*Kwa wao mambo ya cheche*

*Huwa usolidhaniya.*

*64. Kwetu sisi Isilamu*

*Mavazi kitu muhimu*

*Na sisi yatulazimu*

*Ya zipimo kwangaliya.*

Mvulana anapawa upeyo na mipaka ya mambo ya harusi aṭakavoyaenresha na nani aṭakuwa chaṇḍama wake kwenra kuṭowa mkono k̇a kina mke; rafiki yake amekatazwa asenre. Piya kucheza harusi kuwe ni k̇a gharama nrogo na nguwo za bibi yake ziwe ni zile zinazochunga mipaka ya ḍini. K̇a hivo, ḍini inampa mume upeyo wa uṭawala wake katika masikani yake ambako nriye 'mfalume wa nyumba'.

Kuṭokana na msururu wa utʰunaji wa mambo nrani ya masikani piya saa nyengine afanye naye dhihaka k̇a kubishana naye. Ubishani huu uwe si wa maneno mabaya au hasira bali wa kuleta kicheko na furaha k̇a shere aliyomfanyiya. Mtunzi hakuwacha kutupa ukinzanaji huu:

*84. Nena naye kwa dhihaka*

*Afurahi akicheka*

*Mwanamke huudhika*

*Mno kumnyamaliya.*

*85. Mfanyie na ubishi*

*Kwa maneno yaso ghashi*

*Na kwake kuwa mteshi*

*Bila ya kupindukiya.*

Mtunzi anaṁeleza ṁanawe afanye dhihaka lakini si za kukasirisha bali kufurahisha; amfanyiye shere bila ya kuudhi. Na hili la mṭafaruku wa kidhihaka huleta naṭija ya kwonrowa hasira baina yao wawili

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1181

ikiwa zipo k̇a kuleta k̇elezeyana na kurekebishana na kupata maelewano zaiḍi.

Ṁanamke ana mabaḍiliko ya kimaumbile yanayoṭokeya karibu kila ṁezi na saa nyengine mabaḍiliko haya huwa makuḃa zaiḍi anaposhika mimba. Usṭadhi amezipa hali hizi nafasi kubwa katika *Ramanime* kuṭoka beṭi 163 – 185. Anachora ṭaswira ya mtʰu ṭafauṭi ambayo k̇a sasa ameṭoka kuwa ṁenye furaha na bashasha hadi mtʰu ṁenye hasira za mbelembele na ugoyigoyi usojulikana sababu. Anasema mtunzi:

*163. Ifahamu tafauti*

*Waliyo nayo banati*

*Hawezi kuidhibiti*

*Hali inapowadiya.*

*167. Katika siku za ada*

*Ya mwezi hupata shida*

*Ndipo hata na ibada*

*Mungu kawapunguziya.*

*170. Huwa mno ni wakali*

*Nadhani hata akili*

*Haiwi sawa kamili*

*Na punguwani hungiya.*

*174. Kuna na muda wa mimba*

*Mara kwa mara huvimba*

*Ukaona kana kwamba*

*Mekuwa hukuzengeya.*

*177. Zielewe siku hizi*

*Mimba na siku za mwezi*

*Kiwa humbembelezi*

*Taona wamuoneya.*

*178. Mpembe kama kijana*

*Tena aliyo mnuna*

*Ndipo mutasikizana*

*Na yadumu mazoweya.*

Mvulana anafunzwa kimbele kuhusu mabaḍiliko aṭakayokuwa nayo mkewe pinri waowanapo. Kuna ada ya hedhi ambayo humjiya kila ṁezi na ashikapo mimba yake basi kuna misukosuko ya umitʰo na kuileya mimba hiyo. Mabaḍiliko huwa makuḃa mpaka watʰu hushangazwa na hali hiyo. Ṁili hunyong’onyeya, chakula hula k̇a kupʰapiya na saa nyengine walacho hukitapika. Hali zawo hugeuka kuwa wakali pasipo sababu na mara hukuchukiya wewe mume. Juu ya ukʰuu wake anaṭakiwa mume awe na subira k̇a hali zoṭʰe hizo na piya ambembeleze mkewe kama mtoto wake ṭena yule ampeṇḍaye. K̇a hivo cheyo chake cha uḃana kinakuwa cha mtuṁa k̇a mtʰu alobadilika kimaumbile wakaṭi ule.

Katika hali hiyohiyo ya uḃana wa mume anapoingiya nrowani, anashauriwa piya awe na akili makinifu wakaṭi mjaḍala unapoṭokeya masikanini. Kijamii ya waSwahili mume ana saṭwa kubwa mbele ya mke lakini inapofika wakaṭi wa mashauri mume anashauriwa na Usṭadhi aruḍi chini ili wapate kuwafikiyana katika wanaloshinraniya. Na ikiwa kauli ya mke iṭasibu sawa basi yeye mume asikasirike kuwa kauli yake haikupita na akaweka ṭurufu k̇amba nriyo kauli iṭakayotumika na liwe liwalo. Anaonywa kuhusu kutumiya uwezo huwo k̇a sababu mke piya ana haki sawa katika mashauri hayo. Anashauriwa na mtunzi hivi:

*117. Usitake kwa lazima*

*Kula yambo ukisema*

*Alikubali daima*

*Papo hapo kuridhiya.*

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1181

*118. Muatiye makawanda*

*Anene anolipenda*

*Na kwa huja kikushinda*

*Siwe vito tatumiya.*

*120. Kubali mezolinena*

*Umuunge tena sana*

*Na faida utaona*

*Mambo taandama ndiya.*

*121. Na yeye kikasirika*

*Wewe usipande shuka*

*Na akizidi ondoka*

*Kishindwa kuvumiliya.*

Katika mashauriyano ya masikani kawaiḍa asiwe mume nriye msemaji asikize na ṁenziwe. Kauli yake ikiwa imewafiki basi ifuwaṫe na mambo yaṭakuwa mazuri kila wakaṭi. Na anaposhinrwa katika mjaḍala asipanre hasira bali ashuke ili wapatane k̇a jambo hilo.

**Upete**

Tumesema awali kuwa kauli zoṭʰe zinapotʰongolewa basi huṭegemeya mukṭadha wa maneno mengine katika mtʰongoo huwo na maana ya awali yaweza kugeuka na kuja ṭafauṭi—kupeta kiḍogo. K̇a mfano, katika *Ramanime* mume nriye ajulikanaye kuwa fahali na ṁenye mbegu za uzazi lakini ikiṭokeya k̇amba katika kujamiiyana k̇ake hakuna naṭija ya mkewe kushika mimba basi mambo hayo huwa ni siri ya siri (ubeṭi 144) na hayaseṁi waziwazi. Lakini ili kutatuwa shida hii mume anashauriwa aungane na mkewe wenre wakaṭafuṭe dawa ya kasoro hii na iṭakapobiḍi haya maneno ya siri wanakubaliwa kuyaṭowa hadharani, k̇a daktari (ubeṭi 144). Na mume anahimizwa na Usṭadhi asikataye k̇a sababu yaweza kutatuka shida hii.

Mfano ṁengine ni shauri la kuwowa laṭokana na mvuli k̇a hivo yeye nriye nahodha wa kuliyenresha wazo hilo. Na ḍini nayo inaṁambiya kabla hajaowa afanye uṭeuzi wa mke yupi aṁowe. Na kama wasemavo waSwahili ‘kuwowa ni kutiya mkono gizani’ Usṭadhi anamshauri ṁanawe asivurumize mkono ṭu gizani bali afanye uṭeuzi wa kimahesabu. Yaani baḍala ya kujiṫaliya binṭi yoyoṭʰe afanye uṭeuzi kulingana na vipimo fulani na vipimo hivo viwe ni vile va ḍini vilivofafanuliwa na Mtume Muhammaḍ (ubeṭi 11 – 15). Aweza kuwowa mke ṁenye mali, ṁenye nasaba ṭukufu, ṁenye uzuri wa hurilaini lakini yoṭʰe yamefungamanishwa na alo na ḍini. K̇a hivo, ṫaelezwa kuwa mume anawo uhuru wa uṭeuzi lakini analekezwa uhuru huwo autumiye kimahesabu.

Wak̇eze mvuli anaambiwa awape heshima ya hali ya juu na wala asisubuṭu kuwakoseya heshima haṭa mara moja. Lazima awasaiḍiye wazee hawo ikiwa ni watʰu wahiṭajiya msaaḍa wake na awezapo yeye awapelekee msaaḍa huwo. Mtunzi anamkʰokoteza ṁanawe hivi:

*205. Nawe kimpenda mke*

*Wapende wazee wake*

*Wakwe mbwako siepuke*

*Na hishima kuwekeya.*

*208. Wewe katu sisubutu*

*Kudharau hao watu*

*Hata kama utukutu*

*Kwao umeshuhudiya.*

*210. Ukiwa una nafasi*

*La kuwapa sikuwasi*

*Ila fanya kwa kiasi*

*Siye dewe kakutiya.*

*218. Wakiwa ni wahitaji*

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1181

*Siwangoje kutaraji*

*Wakiwa kwako hawaji*

*Ni sawa kuwapekeya.*

Tuṭaona katika beṭi hizo mume anausiwa awapeṇḍe wak̇eze na awaheshimu kama wazazi binafsi. Piya awasaiḍiye katika masurufu yao ya nyumbani na ikiwa aweza awapelekee k̇a sababu wak̇e wengine waona uzitʰo kuomba na wao wana uhiṭaji. Lakini juu ya hayo, Usṭadhi anaṫambiya kuwa ni wale wak̇e wazuri ambawo hawana uso wa kuombanriyo wa kusaiḍiwa ama wak̇e, wajomba, na mashangazi wenye kupeṇḍa kupawa hawo ajiyepushe nawo ṭaratibu bila kugombana nawo (beṭi 219 – 223).

Tukichukuliya kuwa ḍini nriyo msingi wa maisha ya nrowa basi ḍini ya kiIsilamu imekubali mvuli kuwowa zaiḍi ya mke mmoja haṭa katika *Ramanime* limeṭajwa. Dharura za k̇engeza kuwowa zaweza kuwa kama alivozitaja Usṭadhi: mke ana maradhi (ubeṭi 197), hana kizazi (ni tasa) (ubeṭi 198), au mashughuli ya ngono hayawezi (ubeṭi 199). Lakini ikiwa si sababu hizi basi asiowe mke wa zaiḍi asilani. Amemkataza kuwowa mke wa pili, japo ḍini yakubali, si k̇a sababu za kiḍini bali k̇a sababu ya ṭajiriba yake mtunzi maishani alivoyaona mpaka ameita kuwowa mke wa pili, udhiya. Hofu yake mtunzi ni wanawake nriyo wenye shida katika ukewenza: wengine huwa wakali, wengine nriyo ḍawa ya maringo yao k̇a mume lakini sanasana wana viṭimbi visivowezeka kuchukulika. Haṭa hivo, k̇a kucheleya kuṭofanya uwaḍilifu baina ya wake-wenza ḍini imemkataza (Quran, 4:3) mume mmoja kuowa wanawake wawiliwawili au watatuwatatu au wanewane. Kimaoni yetu, Usṭadhi ameleta fasiri nyengine katika masiyala ya kuwowa mke wa pili si k̇a kipimo cha uwaḍilifu bali ametumiya ṭajiriba kupetesha kipimo na kufanya udhiya wa wake-wenza au kuwowa k̇a sababu ya kuwowa ṭu kuwa dharura kʰuu ya kumkataza ṁanawe Yahaya [k̇etu sisi mume yoyoṭʰe] k̇engeza mke.

*193. Mke siowe wa pili*

*Ni udhiya kweli kweli*

*Na ingawa ni halali*

*Ni uzito kutumiya.*

*194. Na wanawake si sawa*

*Kwa wengineo ni dawa*

*Utaiyuta kuzawa*

*Nimekwambiya Yahaya.*

*195. Kuna wanao ridhika*

*Wangawa wanun'gunika*

*Kuna wangine huwaka*

*Fununu wakisikiya.*

*196. Kuongeza si haramu*

*Walakini ufahamu*

*Ni kuu mno jukumu*

*Mbali na wake udhiya.*

*200. Kwa dharura ziso budi*

*Usitende kwa kasidi*

*Kuengeza wa zaidi*

*Kitosheleza mmoya.*

*201. Kwa mmoya kutosheka*

*Ndiyo bora bila shaka*

*Kuengeza ukitaka*

*Ni kama nilokwambiya.*

Mtunzi anamuwasa ṁanawe Yahaya (na katika jambo hili amemṭaja k̇a jina kabisa kwonesha anamlenga yeye) asijaribu kuwowa mke wa pili. Aṭapata ṭaabu kuɓa kuṭoka k̇a wake-wenza. Waṭamfanyiya udhiya wa hali juu mpaka aṭajijuṭiya.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1181

Bora zaiḍi aṭosheke na huyo mmoja asiyengeze kabisa. Yahaya aowe k̇a sababu za kidharura kama tulivoziṭaja lakini asiowe k̇a sababu ya kusudi au kuwowa k̇a sababu ya kuwowa ṭu.

Ufungamanisho wa elimu ya maḍarasani na ṭajiriba ya maisha kupetesha maana inaturegesha katika uṭeṇḍi wenyewe ambapo Usṭadhi anazungumziya masiyala ya Mungu, Mtume, Maswahaba katika uṭeṇḍianawouwita 'nudhuma' ubeṭi 1. Katika mawasiliyano yangu naye 2011 katika uṭafiṭi ṁengine, Lamu, Usṭadhi alinifafanuliya ṭafauṭi iliyopo baina ya isṭilahi 'nudhuma' na 'shairi'. Aliniyeleza k̇amba nudhuma ni utungo ambawo una maelezo ya kutʰuna yanayoegemeya zaiḍi ḍini na shairi ni utungo unawoegemeya k̇enye mambo ya mahaba na ya kikawaiḍa. K̇a kupatikana maudhui ya ngono, mahaba, na ukewenza ṫaweza kusema kuwa Usṭadhi amekhalifu na kupetesha sajili ya nudhuma.

## Mjaḍala

Uchanganuzi wetu wa maṭini ya *Ramanime* umetupa ufafanuzi wa namna mvulana anavokumbana na maisha mapya anapoingiya k̇enye maisha ya nrowa. Tumeona k̇amba jamii ya waSwahili juu ya kuhesabu kʰoo zake kukeni (Chiraghdin, 1977) na baaḍaye kuumeni walipoṭangamana na wageni (Middleton, 1992), humpa cheyo cha juu mvulana na mume. Hadhi hii ya uume nriyo inayomfanya mvulana ajiyone kuwa ana uhuru na uwezo wa kujichaguliya ṁelekeyo wa maisha yake akishaowa. Hadhi hii piya nriyo inayoenrelezwa na jamii kupitiya mafunzo wanayopawa vijana wakiwa jaṇḍoni au unyagoni au wakiwa katika masikani k̇a wazazi wao (Cory, 1947). Hadhi hii hutumiwa na mume k̇ezeka maṭabaka na kujiweka yeye juu ya wengine woṭʰe katika jamii akiwamo mke chini yake. K̇a hivo, ṭangu mwanzo anapawa na jamii uwezo na nguvu za kiyuṭawala ambazo aṭakuja nazo nrowani. Jihazi moja anayoweza k̇itumiya kufaulisha uṭawala wake ni kujishughulisha na mkewe na kutumiya lugha ṭamu kila saa hivo kumteka nyara mkewe kama alivofanya Ṁanakupona kumshauri bintiye amteke mumewe k̇a maneno ṭu (Biersteker, 1991 uk. 74).

Kezilahabi (1991) na Usṭadhi wamekuja kuvunja kasumba hii ya uhadhishaji wa mume katika jamii na kushikiliya kuwa woṭʰe wana majukumu sawa katika k̇enreleza jamii. Kezilahabi k̇enye kurasa 126-7 anasawirisha kuwa lau nuru za watʰu wawili hawa (mume na mke) ziṭashikana na kuwa moja basi ziṭaangaza uliṁengu mzima na ṭangamano la wanajamii woṭʰe (binaḍamu na wanyama) liṭakuwa na amani. Katika *Ramanime* mvuli anapawa uwongozi wa hekima auchukuwe kama ufunuwo wa kuona mbele maisha ya nrowa yaṭakuwaje. K̇anza kabisa *Ramanime* unamvunja mvulana msingi wa uṭegemezi wa akili yake katika uṭeuzi wa mke, kusherehekeya harusi yenyewe, kuṭangamana na marafiki. Hapa unamwonesha kuwa uṭeuzi si wake bali ni wa kigezo cha nje ya maṭako yake. Dini inadhihirishwa kuweka barabara ya kupitiwa kila muumini wa kiIsilamu na hapo hana buḍi kufuwata njiya hiyo. Walakini *Ramanime* inamwonesha kuwa wakaṭi ṁengine aṭatumiya hali ilivo katika suala ibuka na hapo atumiye akili au lipi lililobora kufuwaṫa kama la kumkataza k̇engeza mke wa pili.

Baaḍa ya kumfanya hawezi kujichaguliya ṁenza wa maishani baaḍaye anafunzwa k̇amba katika maisha kila aṭakalofanya ajuwe hayuko peke yake ana ṁenzake. Namna aṭakavozungumza naye, aṭakavoipamba nyumba k̇a sababu ya ṁenzake afurahi, namna aṭakavojipamba yeye ṁenyewe k̇a ajili ṁenzake aone raha apeṇḍeze mbele za watʰu, namna aṭakavoingiliyana naye haṭa katika tenro la kujamiiyana. K̇a hivo, maisha huwa si yake ṭena peke yake bali ni ya watʰu wawili. Katika uwili huu usemezanaji huwa ni mume amfanyiye mkewe kila kitʰu kupata furaha ya mkewe. Na mke naye k̇a kufurahika yeye basi huregesha furaha k̇a mumewe na zaiḍi humpa uṭiifu. Ṁanamke mwenye ḍini hushariṭizwa kuwa mṭiifu ḍaima k̇a mumewe nriyo mume akaambiwa aowe mwenye ḍini.

Maisha hayakupangika kuwa ni msiṭari unaoṭoka kumoja k̇enra k̇engine bali kuna mapetomapeto

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

njiyani yanayohiṭaji wananrowa kuyasairi kivengine kila yanapojichipuza. Haswa mume jukumu la k̇elewa mabaḍiliko ya hali katika nrowa amewachiwa yeye k̇a sababu ameambiwa kila siku asome maisha na amsome ṁenziwe. Ujifunzaji unaṁangukiya mvuli; kila siku yeye ni ṁanafunzi angajiṭaka ni mfalume wa nyumba au ṁalimu wa ḍarasa la masikani yake. Si ajabu katika uchanganuzi wetu tulipata kuwa mume alikaṭazwa asifanye mambo 79 na aliyamrishwa afanye mambo 60 tukichanganya maagizo yoṭʰe haya mvulana aṭakiwa afanye mambo chanya ṭakriban 140 na baḍo kila kukicha yaṭayengezeka. Majukumu hayo aṭayajuwa k̇a kumsoma mkewe kila siku na kila anavoenreleya kumfahamu mkewe basi yuwawa bora zaiḍi katika uṭawala wa masikani yake. Usṭadhi alimpa mwanawe siyasa (hekima siyo ujanja) ya kuweza kutumiya ili kufaulu katika mbinu za k̇enresha masikani jambo ambalo Biersteker (1991, uk. 74) anasema ni kitʰovu katika lugha ya ushairi wa kiSwahili.

Tukishikanisha huwo ujamaa na mageuko ya hali k̇a kila wasaa basi kila siku katika maisha ya nrowa ya mume kuna maana mpya inayojiṭokeza ṭafauṭi kiḍogo na ilivokuwa awali. Hii ni k̇a sababu hali mpya huhiṭaji mambo mapya na mume lazima aweze kutumiya maarifa ya kiṭajiriba lakini piya atumiye na mizani za akili yake. Ajuwe kuwa mambo yapelek̇a na mahesabu, na uwangalizi wa jamaa akaraba piya wahiṭajiya mchujo wenye kuwaṭafauṭisha wahiṭaji na makupe, kujiyoleya wanawake zaiḍi ya mmoja ni jambo la kufikiriwa mara mbilimbili, na zaiḍi, mambo ya siri za masikani haziṭolewi nje haṭa k̇a dharura gani labda hapana buḍi. Haṭa mara nyengine iṭabiḍi aamuwe vengine na msimamo wake wa kiḍini ili naṭija muwafaka ipatikane masikani, kama hilo la k̇engeza mke. K̇a sababu hiyo, mume aweza kuhiṭalifu lililozoweleka k̇a kupanuwa maana k̇amba masuwala yanayozungumziwa ni ya kijamii na mtʰu na ḍini ni katika ujamii. Nriposana, mashekhe na waumini k̇a jumla hujihami na hoja k̇amba masiyala ya nrowa ni ḍini na hakuna kuona haya, kuficha, au tasifida (kama alivofanya Usṭadhi kuzungumziya ngono waziwazi na k̇a kina) katika kuzungumziya ḍini, na msafiri, katika maisha ya nrowa, aweza kuwa kafiri kama msemo unavoshaḍiḍiya.

Ili maisha ya nrowa yasiyonekane ‘maleleji’ mvuli anashauriwa mara nyengine akoroge ule utulivu k̇a kuzuwa ubishi k̇a njia ya dhihaka. Ubishi huu si wa kukasirisha bali ni wa kuleta kicheko ili woṭʰe wafurahike baaḍa ya kupimana akili. Katika mfanyiko huu woṭʰe swali liṭakalozuka ni huyu mume ni nani? Ni mṭawala, ṁalimu, mpenzi, mshangiliyaji mambo masikani, mkulima wa shamba la uzazi, askari wa kuchunza mke, mleta vichekesho, mkufurishaji, au ni mjinga anayeambiwa afuwate ḍini, ṭajiriba, au akufuru azipinge zoṭʰe hizo, afuwate akili yake na saa nyengine asiifuwate akili. Bakhtin (1981 uk. 161) anasema hii ni hali ya kimaharajani ambapo mhusika [mume] anavaa barakowa na hatujuwi yeye ni nani, anapitisha ujumbe wake kisitiyara na kuṭaharukisha kawaiḍa iliyopo hapo kusababisha maana mpya. Nriposana, mume anapoulizwa njiyani, “Jamaa hawajambo nyumbani?” huwa auliziwa mkewe, nruguze, babake, au mamake? K̇enye mukṭadha huu auliziwa mkewe nriyo maana mpya ya ‘jamaa’ nrowani.

## HIṬIMISHO

Lengo la makala haya lilikuwa kuushuwa uṭenḍi huu *Ramanime* katika ṭaaluma ya kiSwahili k̇a sababu, k̇a ufahamu wetu, ulikuwa haujaṭafasiliwa kokoṭʰe. Pili, ni kudhihirisha namna Usṭadhi alivogeuza maana ya cheyo cha mume kuṭoka kuwa ‘mfalume’ anayeamrisha na k̇amuwa kila kitʰu apendeleyavo yeye mpaka kuwa ‘mshirika’ kufu moja na mkewe katika masikani yao. Tumedhihirisha kuwa kama kauli zilivo katika masemezano na zina mabaḍiliko ya kila mara na hivo kupata maana mpya kila kukicha basi na maisha ya nrowa nayo hali kadhalika yamo katika masemezano na jamii nzima ya masikani ya wananrowa, na kila kukizuka masiyala nrowani basi huṭafuṭwa masuluhisho mapya yenye kuwafiki hali

hiyo. K̇a sababu hiyo basi, mvuli anapoingiya k̇enye nrowa afute na asahau akilini ṁake kuwa yeye nriye bosi na ṁenziwe ni kiḏeḏe kiso hisi wala kisi. Chembelecho waSwahili, k̇enye uṭeṇḍi huu Usṭadhi ameyishukisha bendera ya mume.

## SHUKURANI

Asanṭa yangu kʰuu imfikiye Usṭadh Mahmouḍ Ahmaḍ Abdulqadir (Mau) k̇a kuniṭunuku miswaḍa yake miwili (*Ramanike & Ramanime*) nilipokuwa Lamu (2007—2012). Piya iwaenree (Mstaafu) Mbarak Abdulkadir, Aḍam Bakari na Shekale Ṭauzy wa Makumbusho ya Lamu. Nyoṭʰe Jazakumullahu khairaa.

Makala haya nawatabarukiya walimu wangu Ṭima Omari Suwo (f. 2023) na Noor Abeiḍ (f. 2020). WALINIFUNZA MENGI KUHUSU NROWA, NAWASHUKURU.

## MAREJELEO

Abdulkadir, M. A., & Frankl, P. J. L. (2013). ‘Kiswahili’: A poem by Mahmoud AhmadAbdulkadir. Katika *Swahili Forum 20*, 1—18.

Abdulqadir, M. A. (2004). *Utenzi wa ramani ya maisha ya ndoa (mke)*. Mswada haujachapishwa. Lamu.

Abdulqadir, M. A. (2004). *Utenzi wa ramani ya maisha ya ndoa (mume)*. Mswada haujachapishwa. Lamu.

Ankal, N. N. (2013, April 30). *Burudikeni na utenzi wa ramani ya maisha ya ndoa (mke)*. Facebook. https://tinyurl.com/mtue932h

Baalbaki, R. (1995). *Al Mawrid: A modern Arabic-English dictionary*. Dar El-Ilm Lilmalayin.

Bakhtin, M. M. (1981). *The dialogic imagination*. M. Holquist (mh.). The University of Texas Press.

Biersteker, A. (1991). Language poetry and power: A consideration of “Utendi wa Mwanakupona”. Katika K. W. Harrow (mh.) (1991) *Faces of Islam in African literature* (59—78). Heinamann Educational Books.

Bwanalemba, M. (1662). Das geheimnis der geheimnisse [Uṭeṇḍi wa siri li asrari]. Katika P. E. Dammann (1940). *Dichtungen in der Lamu mundart des Suaheli Band 28*. Freiderichesen.

Chiraghdin, S. (1987). *Malenga wa karne moja*. Longman Kenya.

Chiraghdin, S., & Mnyampala, M. (1977). *Historia ya Kiswahili*. Oxford University Press.

Cory, H. (1947). Jando. Part I: The Constitution and Organization of the Jando. Katika *The Journal of the Royal Anthropological Institute of Great Britain and Ireland 77*(2), 159—168.

Jamiiforums.com (2008, August 13). https://tinyurl.com/2d8jdv59 Ilisoṁa 23/02/2023

Kezilahabi, E. (1991). *Mzingile*. Vide~Muwa Publishers Limited.

Mazrui, A. & Njogu, K. (2022). *Mikondo ya Kiswahili: Siasa, jamii na utandawazi*. Twaweza Communications.

Mazrui, A. & Shariff, I. N. (1993). *The Swahili: Idiom and identity of an African people*. Africa World Press, Inc.

Mbaabu, I. (1985). *Utamaduni wa Waswahili*. Kenya Publishing & Book Marketing Co. Ltd.

Middleton, J. (1992). *The world of the Swahili: An African mercantile civilization*. New Haven/London: Yale University Press.

Mohamed, S. A. (2016). *Mashetani wamerudi*. Spotlight Publishers (EA) Limited.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1181

Momanyi, C. (2019). *Nguu za jadi*. Queenex Publishers.

Mwamzandi, I. Y. (2018). Dhana ya zubu katika nyimbo za harusi za Waswahili: Uchambuzi wa kisaikolojia changanuzi. Katika *Mulika 37*, 45—58.

Nabhany, A. S. (h.t.). *Manukato ya Wambeja*. Mswada haujachapishwa. Mambasa.

Raia, A., & Vierke, C. (wah.) (2023). In this fragile world: Swahili poetry of commitment by Ustadh Mahmoud Mau. Katika *Islam in Africa, 25*, 1—396. https://brill.com/edcollbook-oa/title/62192

Shitemi, N. L. (2010). *Mashairi ya kabla ya karne ya ishirini*. Moi University Press.

Wandera-Simwa, S. P. (2021). Mwanamke wa Kiswahili katika utenzi wa Mwanakupona. Katika *East African Journal of Swahili Studies 4* (1), 82—98. https://doi.org/10.37284/jammk.4.1.422

Werner, A., & Hichens, W. (1934). *The advice of Mwanakupona upon the wifely duty*. Azania Press.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.